**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,**
Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu anayetujaalia, uzima na afya tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Kumi na Nane kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, nichukue fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii adhimu na muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda yanayojumuisha utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2020/2021. Namshukuru Allah kwa kutuwezesha sote kusheherekea kwa salama Skukuu ya Eid el Fitri kufuatia kumalizika mfungo Mtukufu wa mwezi wa Ramadhani na nazidi kumuomba Mwenyezi Mungu atukubalie maombi na swaumu zetu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda Balozi Amina Salum Ali na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh maarufu Diaspora kwa umahiri, uzoefu na umakini wao wa hali ya juu waliyouonesha katika kipindi cha kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Vile vile, tunawashukuru watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano waliyotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Kamati hususan wakati wa kuipitia bajeti ya Wizara hii ya Biashara na Viwanda. Kamati inaipongeza sana Wizara kwa kufanya kazi kwa pamoja na kuwa na 'spirit ya collective responsibility'. Huo ndio msingi mzuri wa uwajibikaji.

**Mheshimiwa Spika,**
Shukurani za pekee nazitoa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa ujasiri na umakini wao wa kupigiwa mfano waliyouonesha katika kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2020/2021 na hatimae kuipitisha pamoja na marekebisho madogo madogo waliyoyapendekeza kwa nia ya kuimarisha zaidi utendaji wa Wizara. Kwa heshima kubwa napenda kuwataja Wajumbe pamoja na Makatibu wa Kamati yetu kama ifuatavyo:-

1. Dkt. Mwinyihaji Makame - Mwenyekiti;
2. Mheshimiwa Hamida Abdalla Issa - M/Mwenyekiti;
3. Mheshimiwa Mussa Ali Mussa - Mjumbe;
4. Mheshimiwa Mohammed Mgaza Jecha - Mjumbe;
5. Mheshimiwa Ahmada Yahya Abdulwakil - Mjumbe;
6. Mheshimiwa Nadir Abdul- latif Yussuf - Mjumbe;
7. Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe;
8. Ndugu Asma Ali Kassim - Katibu; na
9. Ndugu Said Khamis Ramadhan - Katibu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kabla ya kuyapitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda kama inavyoelekezwa na Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016. Kiujumla, Kamati yetu imekubaliana na utekelezaji wa miezi tisa wa Wizara hii pamoja na Mwelekeo wa Bajeti yake. Hata hivyo, Kamati yetu haikuacha kutoa ushauri na mapendekezo machache kwa mafungu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii na kwa nia ya kuimarisha zaidi utekelezaji wa bajeti tunayoendelea nayo pamoja na mwelekeo wa bajeti mpya ya mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa mwaka 2019/2020, Wizara ya Biashara na Viwanda ilipangiwa kukusanya jumla ya 1,895,963,000/- ambapo hadi kufikia Machi 2020, Wizara hiyo ilipangiwa kukusanya jumla ya 1,467,159,230/- na kufanikiwa kupata jumla ya 600,133,891/- milioni sawa na asilimia 41 ya makadirio ya makusanyo kwa miezi tisa. Kwa mantiki hiyo, asilimia 59 ya makadirio ya makusanyo hayajafikiwa kupitia vyanzo ambavyo Wizara inavitumia kupata mapato yake.

**Mheshimiwa Spika,**
Kimipango, hali hiyo haitoi taswira nzuri kwa vile inaonekana wazi mipango ya makusanyo iliyowekwa hailingani na uwezo halisi wa makusanyo yanayopatikana. Kwa hali hiyo, kuna kila sababu kwa Wizara ya Fedha na Mipango kutathmini ipasavyo vyanzo vya mapato vya Wizara, uwezo halisi wa makusanyo pamoja na kiwango cha fedha kinachokisiwa kukusanywa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Sisi sote mashahidi kwamba nchi yetu ina malengo mazuri iliyojipangia ya kufikia uchumi wa viwanda utakaotunyanyua hapa tulipo na kutuweka katika uchumi wa kati utakaotuwezesha kujitegemea kwa asilimia kubwa katika mipango, makusanyo na matumizi ya fedha zetu wenyewe. Baada ya kupitia bajeti ya maendeleo na matumizi ya Wizara hii, Kamati yetu imegundua kwamba Wizara ina mipango mizuri ikiwemo uanzishwaji wa maeneo ya maonesho ya biashara na maeneo ya viwanda yaliyopo Nyamanzi, Dunga, Nungwi na Chamanangwe, lakini utekelezaji wake umebakia kinadharia na sio kivitendo. Hali hiyo inaonekana wazi kupitia Bajeti ndogo ya fedha za maendeleo ya shilingi milioni 15,000,000/- iliyopangwa kutumiwa na Wizara hii kwa mwaka unaokuja kwa ajili ya kuendeleza uwanja wa maonesho wa kimataifa Zanzibar uliopo Nyamanzi ambazo ni fedha kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya ujenzi wa miundombinu katika eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na kuwepo kwa janga hili la maradhi ya Covid - 19, lililopelekea uchumi wa nchi yetu unaotegemea zaidi utalii kuelekea kuanguka kwa vile ndio sekta kuu tunayoitegemea kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi wa nchi yetu, Kamati yetu inaishauri Serikali ijikite ipasavyo na uendelezaji sekta nyengine hususan viwanda

na kilimo, Kamati inaamini kwamba iwapo tungeandaa mazingira ya kuzikuza kikamilifu sekta hizo zingetunyanyua na kupunguza makali ya mwelekeo wa anguko hilo kwa kufanya mzunguko wa fedha kwa wananchi wetu kuimarika zaidi na kusaidia mapambano dhidi ya maradhi hayo kwa vile bidhaa kama vitakasa mikono (sanitizer) na hata nguo za madaktari wetu zingeweza kutengenezwa kwa wingi kupitia viwanda vyetu vya ndani na bidhaa nyengine tungeweza kuziuzwa hata nje ya nchi yetu. Kwa mantiki hiyo, kuna kila sababu kwa sekta ya kilimo, utalii na viwanda kupewa kipaumbele ulio sawa ili sekta moja ikianguka iweze kunyanyuliwa na sekta nyengine.

**Mheshimiwa Spika,**
Suala zima la kuwepo takwimu sahihi za biashara inayofanyika nchini ni la msingi kuimarishwa kinyume na hivyo mipango katika uendelezaji biashara haitoweza kuakisi hali halisi ya biashara inayofanyika. Kamati yetu imegundua kwamba kuna changamoto kubwa ya kutopatikana takwimu nyingi za biashara hususan katika Bandari bubu pamoja na Bandari ya Mkokotoni. Matokeo yake, mipango ambayo Wizara hupanga huwa na kasoro nyingi ndani yake ikiwemo kukosa kutambua mahitaji kamili na sahihi ya bidhaa zinazohitajika ama kutumika Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yetu inaipongeza Wizara kwa kukamilisha kilio chake cha siku nyingi kilichopelekea kukamilika kwa maandalizi ya kuanzishwa kwa Sheria ya Wakala wa Vipimo na sasa tayari imeshawekwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ni matumaini ya Kamati yetu kwamba Sheria hiyo itakuwa mkombozi kwa wananchi na wafanyabiashara wetu kwani wataweza kupata bidhaa sahihi kulingana na mahitaji ya thamani halisi ya fedha zao kwa vile kitengo kitakuwa kinafanya kazi kama Wakala na kuongeza wigo zaidi wa ukaguzi wa mezani na vipimo. Sambamba na hilo, Serikali yetu itaongeza mapato yake maradufu kupitia Wakala huu kutokana na kuanza ukaguzi katika maeneo tofauti ambayo kwasasa bado hawajayafikia yakiwemo ukaguzi wa bidhaa zinazofungashwa na ujazo wa magari ya mchanga pamoja na ukaguzi wa vipimo vya dhahabu ambavyo Wizara imevigundua kuwa na udanganyifu mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yetu inaendelea kukishauri kitengo cha Mezani na Vipimo kibadilike kikamilifu mara tu baada ya kuwa Wakala kwani kuna maeneo mengi ambayo hawajayafanyia kazi na kutuongezea mapato mengi katika makusanyo ya Wizara

Kadhalika, Kamati yetu inazitaka Taasisi nyengine za Serikali zikiwemo ZURA na ZBS kufanya kazi kwa mashirikiano ya karibu na Wakala huu kinyume na hivyo utekelezaji wa majukumu ya Wakala huu utabakia ndani ya sheria bila ya kuwepo utendaji.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yetu inatoa pongezi kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) kwa utekelezaji mzuri wa kazi zake kwani kwa miezi tisa imefanikiwa kutoa uelewa kwa jamii kuhusu dhamana na kazi zake hasa ukizingatia utaratibu wa usajili umebadilika kutokana na matumizi ya mfumo maalum na wa kisasa wa usajili. Aidha, Wakala huo umefanikiwa kusajili makampuni 636, majina ya biashara 884 na nyaraka 791 pamoja na kuandaa rasimu ya marekebisho ya sheria ya ufilisi (insolvency). Kamati yetu inautaka Wakala kukamilisha marekebisho hayo haraka iwezekanavyo ili mswada huo uweze kuwasilishwa Barazani na Waheshimiwa Wajumbe watakaojaaliwa kuwemo katika Baraza lijalo waweze kuupitisha.

**Mheshimiwa Spika,**
Katika hatua ya kuviendeleza viwanda pamoja na Wajasiriamali wetu nchini, SMIDA tayari imeshaandaa Kanuni na muongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati pamoja na muongozo wa mafunzo kwa wazalishaji wetu. Kadhalika, SMIDA imefanikiwa kuwainua na kuwaendeleza wajasiriamali wetu ili waweze kufanya kazi zao katika mazingira mazuri kwa kuwapatia mikopo yenye thamani ya shilingi 100,000,000/-. Kamati yetu inaamini kwamba wajasiriamali wetu wanao ujuzi wa hali ya juu isipokuwa changamoto kubwa inayowakabili ni ukosefu au upungufu wa mitaji. Hivyo, juhudi za mikopo nafuu kwao itaweza kuwatoa katika hali duni ya uzalishaji inayowakabili na kukuza uzalishaji wao kwa kuziongezea thamani bidhaa zao.

**Mheshimiwa Spika,**
Suala la uimarishaji wa viwango vyetu vya ndani ni jambo la msingi kufanyiwa kazi na Wizara ya Biashara na Viwanda kwani kadiri nchi yetu inapoviidhinisha viwango ndio inatanua wigo wa usalama wa wananchi wetu kupitia vifaa au bidhaa wanazozitumia. Kamati yetu inaipongeza Wizara kupitia Taasisi yake ya Viwango (ZBS) kwa kulifanyia kazi kivitendo suala hilo kwani tayari imeshaandaa na kuidhinisha viwango 104 vya bidhaa za uhandisi, kemikali, vyakula, mboga, mbolea na dawa za kuulia wadudu pamoja na kutoa alama saba za ubora kwa jumuiya tofauti. Kamati yetu inaisisitiza Wizara kuhakikisha viwango

wanavyoviandaa viwe sahihi na viendane na kukubalika na Taasisi za viwango za kimataifa hasa ukizingatia kwamba ulimwengu hivi sasa umekuwa kama kijiji kimoja. Iwapo hilo litafanikiwa, bidhaa ambazo zimepatiwa viwango na alama za ubora Zanzibar zitaweza kutambulika na kutumiwa na mataifa mengine ulimenguni.

**Mheshimiwa Spika,**
Juhudi za kuendeleza uchakataji wa mazao yenye mafuta (oil crops) kwa lengo la kuzalisha mafuta linatakiwa kuendelezwa ili liweze kuongeza uzalishaji wa mafuta maalum nchini, Kamati yetu inakubaliana na mpango uliopo unaoendelezwa na Wizara kupitia Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) wa kukifanyia matengenezo makubwa kiwanda cha uzalishaji wa mafuta ya Makonyo na Arki kiliopo Wawi Pemba. Hata hivyo, Kamati yetu imepata wasiwasi wa kutokuwepo kwa malighafi ya makonyo ya kutosha yatakayotumika kuendesha kiwanda hicho. Wizara iongeze juhudi kuwasaidia wakulima wetu ili waweze kupanda mikarafuu zaidi kwa vile mikarafuu inayotegemewa kwa uzalishaji hivi sasa mingi yao ni mikongwe ambayo uzazi wake umepungua kwa kiasi kikubwa. Kamati yetu inaamini uzalishaji wa karafuu na makonyo Zanzibar unaweza ukatosheleza mahitaji ya kiwanda cha makonyo kwa vile bado kuna maeneo mengi hayajapandwa mikarafuu na ardhi yake ni rafiki mno kwa uzalishaji wa rasilimali hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**
Migongano ya kiutendaji kati ya Wizara hii na Wizara ya Kilimo hususan katika masuala ya ukulima wa mwani na uendelezaji wa mazao ya kibiashara kama Karafuu, Iliki na mazao mengine ya viungo hapana budi yapatiwe ufumbuzi wa kudumu. Aidha, viwanda vinavyohitaji mazao kwa kuchakatwa (agro-proccessing) lazima viwekewe msingi mzuri kutoka Wizara ya Kilimo kama vile Kiwanda cha Maziwa na Sukari.

**Mheshimiwa Spika,**
Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ni chombo muhimu ambacho kikitumiwa ipasavyo kitawalinda wananchi wetu dhidi ya udanganyifu na hila za baadhi ya wafanyabiashara wasio na uaminifu kwa kuzifanyia ukaguzi bidhaa au vifaa vinavyoingizwa nchini ili viendane na viwango vilivyowekwa na kukubalika nchini. Kwasasa, Taasisi hiyo inaendelea na kazi za Ujenzi wa Ofisi, ununuzi wa vifaa vya maabara pamoja na kujenga uwezo wa watendaji wake. Ni busara kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuipatia bajeti ya kutosha ili taasisi hii iweze kujiendesha na kujitegemea ipasavyo kimapato kama zilivyo taasisi nyengine za

aina hiyo. Hata hivyo, Kamati yetu inaipongeza Serikali hususan Mheshimiwa Rais wetu kwa msimamo wake ulio thabiti wa kuipatia fedha Taasisi hii zilizopelekea kununua baadhi ya vifaa muhimu vya kupima ubora wa mafuta ya petroli na desiel ambavyo vimegharimu fedha nyingi.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yetu inaishauri ZBS kupitia Mradi wake wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar ambao kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umepangiwa jumla ya shilingi bilioni 3,000,000,000/- zikiwemo fedha za ununuzi wa vifaa vyengine vya maabara, Kamati yetu inaiomba Serikali fedha hizo zipatikane ili iweze kujikita na ununuzi wa vifaa vya kupima mafuta ya vilainishi vya gari na vifaa vya ujenzi kwani kuna udanganyifu mkubwa unaofanyika na kuwagharimu fedha nyingi wananchi wetu.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa umakini na usikivu wao wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii. Kwa vile Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda, naomba Sasa nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili waichangie, waijadili, waihoji na hatimae kuipitisha kwa kuiunga mkono bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kusema hayo, Kwa niaba ya Mwenyekiti na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………..,
Mheshimiwa Ahmada Yahya Abdulwakil,
Kny: Mwenyekiti,
Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**